

## **HOTUBA YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI KATIKA BARAZA MADIWANI LA ROBO YA PILI TAREHE 16.01.2017.**

### **1. SHUKRANI**

**Ndugu wananchi,**

Awali ya yote napenda kumshukuru MUNGU kwa kutuwezesha kufika mwaka mpya wa 2017. Heri ya mwaka mpya. Katika robo hii ya pili inayoanza mwezi Oktoba hadi Desemba katika mwaka wa fedha 2016/17 tumetekeleza mambo kadha wa kadha katika sekta mbalimbali kama vile;

1. Kuanza ujenzi wa ofisi ya makao ya Halmashauri,
2. Kuanza ujenzi wa stendi,
3. Ukarabati wa miundo mbinu na ujenzi wa majengo mapya maeneo mbalimbali hasa katika sekta ya afya,
4. Kuboresha sekta ya kilimo na mifugo na
5. Kuboresha suala la elimu.

### **2. MIRADI YA MWAKA 2016/17**

**Ndugu wananchi,**

Hadi kufikia tarehe 31.12.2016 kwa robo ya pili, Halmashauri ilikuwa imepokea **Tsh 2,228,177,416/=** kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, na kutumia Tsh 977,469,460/= sawa 43.87% ya fedha zilizopokelewa. Pia Halmashauri imepokea fedha nje ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka 2016/2017 kiasi cha Tsh **260,173,468/=** zikiwa ni fedha za mfuko wa barabara (rollover fund) kwa ajili ya kulipa kazi za barabara zilizotendwa 2015/2016 ambazo fedha yake ilikuja kidogo na Tsh **147,193,468/=** sawa **56.58%** zimekwishatumika kwa kulipa Wakandarasi waliomaliza kazi kwa mujibu wa mkataba.

#### **2.1 KUANZA UJENZI WA OFISI ZA MAKAO YA HALMASHAURI,**

**Ndugu wananchi,**

Tayari tumeanza ujenzi wa ofisi za Halmashauri ambapo hadi sasa majengo yamefikia hatua ya kupauliwa na kutumuia gharama zaidi ya milioni 300 ambapo ujenzi unategemea kukamilika mwezi Februari 2016. Ndugu wajumbe tayari Srerikali imeleta fedha nyingine Tsh.milioni 600 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Halmashauri kwa awamu ya pili na Tsh.milioni 150 kwa ajili ya nyumba ya Mkurugenzi na tayari taratibu za zabuni zimeanza ili kazi itangazwe. Lengo letu ni kuhakikisha ujenzi wa awmu ya kwanza unapoisha mwezi Februari basi awamu ya pili inaanza ili ikiwezekana mwaka huu 2017 tukamilishe ujenzi wa wing moja na kuanza kuhamia Kanyamfisi.

## **2.2 UJENZI WA STENDI**

**Ndugu wananchi,**

Tayari tumeanza ujenzi wa stendi kwa eneo kusafishwa, barabara kuchongwa, kifusi kumwagwa na kuanza kuchimba shimo la choo. Lengo letu tunataka tuanze kutumia stendi mpya ili kuinua kiwango cha mapato. Aidha uwepo wa stendi utaongeza wigo wa ajira kwa wananchi wetu kwani watapewa vibanda ambavyo ni zaidi ya 100 na kufanya biashara wakati huo huo Halmashauri ikipata mapato.

## **2.3 UKARABATI WA MIUNDO MBINU NA UJENZI WA MAJENGO MAPYA**

**MAENEKO MBALIMBALI HASA KATIKA SEKTA YA AFYA,**

**Ndugu wananchi,**

Katika robo hii ya pili, Halmashauri kupitia wataalam wake imeandika maandiko mbalimbali na kufanya mazungumzo na wahisani ambao wamekubali kutudhamini katika miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa wodi ya wanaume na wanawake na maabara katika kituo cha afya Nyanzige ambapo tayari majengo yamepauliwa na usafi unafanyika. Aidha Serikali ilitoa Tsh.milioni 10 ili kukarabati Zahanati zilizopo Kakonko. Vilevile shirika la Engender Health linajenga maternity wing katika Zahanati 4 za Kabingo, Kazilamihunda, Katanga na Nyabibuye. Lengo kubwa na kuboresha hali ya afya katika Wilaya yetu.

## **2.4 KUBORESHA SEKTA YA KILIMO NA MIFUGO**

**Usambazaji wa pembejeo**

**Ndugu Wananchi,**

Usambazaji wa pembejeo zenye ruzuku ya Serikali zilifika tarehe 3/12/2016 na kuanza kusambazwa vijijini tarehe 12/12/2016 baada ya mgao kwa vijiji 44 ndani ya Wilaya ya Kakonko uliofanywa na Kamati ya Pembejeo ya Wilaya. Katika mgao huo kila kijiji kilipata mgao wa mifuko arobaini (40) isipokuwa kijiji cha Nyakayenzi na Kinonko ambavyo vilipata mifuko sitini (60) kila kimoja. Hadi Kufikia tarehe 04/01/2017 jumla ya tani 77.45 (mifuko 1549), kati ya tani 90 (mifuko 1,800) za mbolea ya kukuzia (UREA) imefikishwa katika vijiji 42 kati ya vijiji 44.

**Mlipuko wa ugonjwa wa Chambavu**

**Ndugu Wananchi,**

Katika robo hii ya mwaka kulitokea ugonjwa wa Chambavu kwa wanyama ambapo jumla ya ng'ombe 703 walichanjwa na ng'ombe 113 walikufa. Na hii ni kutokana na baadhi ya wafugaji kutofuata maelekezo ya wataalam na kununua dawa maeneo mengine na kuchanja mifugo yao lakini dawa hizo kutofanya kazi. Hata hivyo tumedhibiti ugonjwa huo na hali ni shwari kwa sasa.

## **2.5 KUBORESHA SUALA LA ELIMU.**

**Ndugu wananchi,**

**Ufaulu kwa watahiniwa wa darasa la saba -2016:**

Jumla ya Watahiniwa **1391** walichaguliwa kuijunga kidato cha kwanza katika Shule za sekondari za ndani na nje ya Mkoa wa Kigoma, Kati ya Watahiniwa hao, Wavulana walikuwa **708** na Wasichana ni **683**, hivyo kufanya Asilimia ya ufaulu kuwa ni **76** na kuifanya Wilaya ya Kakonko kuchukua nafasi ya **Tatu (3)** Kimkoa. Aidha watahiniwa Saba (7) walichaguliwa kuijunga na Sekondari za nje ya Mkoa, kati yao wavulana ni 5 na wasichana ni 2.

**MWISHO.**